

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU**

Simu: 255-262961500/1
Nukushi: 255-262961502
Baruapepe : press@ikulu.go.tz
Tovuti : www.ikulu.go.tz



OFISI YA RAIS,
IKULU,
1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,
CHAMWINO,
S.L.P 1102,
40400 DODOMA.

Dodoma
01 Februari, 2024

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

RAIS SAMIA AWATAKA WADAU WA SHERIA KUTENDA HAKI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan ameitaka Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na wadau wa usuluhishi kubainisha maeneo yanayotakiwa kufanyiwa kazi ikiwemo kutunga sera ya usuluhishi.

Rais Samia amesema hayo leo wakati akihutubia katika maadhimisho ya siku ya sheria nchini yaliyofanyika kwenye viwanja vya Chinangali.

Aidha, Rais Samia amesema ni wakati muafaka wa kujielekeza kufanya utatuzi kwa njia ya usuluhishi bila kufungwa na masharti ya kiufundi yanayokwamisha kutenda haki.

Rais Samia pia ameitaka Wizara ya Katiba na Sheria kwa kushirikiana na wadau kutekeleza kikamilifu utoaji wa msaada wa kisheria kwa kuzingatia Ibara ya 107A ya Katiba inayowataka kutenda haki kwa wote bila ya kujali hali zao za kijamii au kiuchumi.

Vile vile, Rais Samia amesema mitazamo ya wadau wa Mahakama nchini haina budi kujielekeza kwenye kupunguza muda unaotumika kwenye mashauri ili wananchi watumie muda wao mwingi kwenye uzalishaji mali.

Rais Samia amesisitiza kuwa ni vyema Mahakama ikatoa kipaumbele cha kuharakishwa usikilizwaji wa kesi za kibiashara katika masuala ya kisheria pindi inapotokea migogoro ili kuvutia mitaji na uwekezaji na kufungua fursa za biashara.

Rais Samia amebainisha kuwa serikali inafanya jitihada kuimarisha upatikanaji wa huduma za kisheria kwa wananchi wasio na uwezo kupitia *Mama Samia Legal Aid Campaign* kwa kuwa kuna uhitaji mkubwa wa msaada wa kisheria nchini.

Kampeni hiyo tayari imewafikia wananchi 383,293 katika Mikoa 6 ya Dodoma, Manyara, Shinyanga, Ruvuma, Simiyu na Singida ambapo imeweza kutatua migogoro takriban 511.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Zuhura Yunus'.

Zuhura Yunus
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu

